



# NISHATI

HABARI ZA  
NISHATI


## News *Bulletin*

[www.nishati.go.tz](http://www.nishati.go.tz) [Wizara ya Nishati](#) [wizara\\_ya\\_nishati\\_tanzania](#) [@Nishati2017](#) [Wizara ya Nishati](#)

Toleo Namba 38

Mei 1 - 31, 2022

# MIRADI YA UMEME WA UPEPO SINGIDA KUKAMILIKA 2023-2027



*Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato*



**LIMEANDALIWA NA KITENGO CHA  
MAWASILIANO SERIKALINI, WIZARA YA NISHATI**

Wasiliana nasi kwa simu namba +255-26-2322018 Nukushi +255-26-2320148 au  
Fika Ofisi ya Mawasiliano, Mji Mpya wa Serikali Mtumba, S.L.P 2494, Dodoma



## BODI YA UHARIRI

**Mwenyekiti**  
**Mhandisi Felchesmi Mramba**  
Katibu Mkuu

**Makamu Mwenyekiti**  
**Kheri Mahimbali**

**Mhariri**  
**Dorina G. Makaya**

### Waandishi

Teresia Mhagama  
Zuena Msuya  
Hafsa Omar  
Timotheo Mathayo

### Msanifu Kurasa

Lucas Gordon

Wasiliana nasi kwa simu  
namba +255-26-2322018  
Nukushi: +255-26-2320148  
au

Fika Ofisi ya Mawasiliano  
Mitumba Dodoma,  
S.L.P 2494, Dodoma



 [www.nishati.go.tz](http://www.nishati.go.tz)

 [Wizara ya Nishati](#)

 [@Nishati2017](#)

 [wizara\\_ya\\_nishati\\_tanzania](#)

 [Wizara ya Nishati](#)

## Miradi ya Umeme wa Upepo Singida kukamilika 2023-2027



*Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato*

### **Na Zuena Msuya, Dodoma**

**N**aibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato amesema utekelezaji wa miradi ya kufua

umeme kwa kutumia nguvu ya upepo katika Mkoa wa Singida inatarajiwa kukamilika kati ya mwaka 2023 na 2027.

Miradi hiyo inatekelezwa na wawekezaji binafsi wenye nia ya kuzalisha umeme na kuliuzia

Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO).

Wakili Byabato alisema hayo, wakati wa kipindi cha maswali na majibu, bungeni jijini Dodoma, Aprili 13, 2022, akijibu swali la Mhe. Jesca Kishoa, Mbunge wa Viti Maalum aliyetaka kufahamu utekelezaji wa mradi huo mkoni Singida.

Katika majibu yake, Naibu wa Waziri wa Nishati alieleza kuwa miongoni mwa miradi hiyo, ni mradi wa kuzalisha umeme wa megawati 50 kwa kutumia nguvu ya upepo, utakaotekelezwa na Kampuni ya Upepo Energy, katika eneo la Msikii, Halmashauri ya Singida Vijijini.

Majadiliano ya mkataba wa kuuziana umeme (Power Purchase Agreement), kati yake na TANESCO yanaendelea.

Wakili Byabato alisema kuwa, mradi mwingine wa megawati 300 utatekelezwa na Kampuni ya GEO Wind ambao unahusu ujenzi wa mitambo ya kufua umeme katika eneo la Kititimo, Halmashauri ya Singida mjini.

Majadiliano baina ya Mwekezaji na mfadhili Green Climate Fund (GCF) yanaendelea.

Pia, alisema mradi mwingine wa tatu ambao ni wa ubia kati ya Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) na Kampuni ya Abu-Dhabi (Masdar) utazalisha Megawati 100, katika eneo la Ikungi, Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi.

## Megawati 200 za Jotoardhi kuzalishwa kabla ya mwaka 2025

**Na Teresia Mhagama, Mbeya**

**S**erikali imesema kuwa, Tanzania itazalisha umeme wa kiasi cha megawati 200 zinazotokana na Jotoardhi kabla ya mwaka 2025.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba, alisema hayo wakati wa ziara yake ya kukagua vyanzo vya nishati ya Jotoardhi vya Kiejo-Mbaka na Ngozi mkoani Mbeya.

Alisema kuwa, Tanzania ina jumla ya maeneo 52 yanayoweza

kutoa nishati ya Jotoardhi ambayo tayari yameshatambuliwa.

Alieleza kuwa, kwa ujumla, Serikali ina mpango wa kuongeza megawati 1100 zinazotokana na Nishati Jadidifu kabla ya mwaka 2025 na hizo megawati zitatokana na vyanzo mbalimbali kama vile Jotoardhi, Jua na Upepo.

Aliongeza kuwa, Wizara ya Nishati inaweka nguvu kubwa katika kuendeleza vyanzo vya nishati ya Jotoardhi kwa sababu vyanzo hivyo haviishi na hivyo ukaguzi alioufanya katika maeneo hayo ya Jaothemo utasaidia



*Katibu Mkuu, Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba akigusa maji ya moto yanayotoka katika kisima kifupi cha utafiti cha Jotoardhi kilichochoorongwa katika eneo la Kiejo-Mbaka wilayani Rungwe mkoani Mbeya. Kulia kwake ni Kaimu Meneja Mkuu wa Kampuni ya Uendelezaji wa Jotoardhi Tanzania (TGDC), Mhandisi Mathew Mwangomba.*

Serikali kuona hatua stahiki za kuchukua ili kuendeleza vyanzo hivyo.

“Kipindi cha ukame maji yanaweza kupungua, lakini Jotoardhi katika kipindi cha ukame au mvua, mvuke unaotoka chini ya ardhi uko palepale.”

Alisema Katibu Mkuu Alisema kuwa, nchi ya Kenya ina zaidi ya megawati 1100 zinazotokana na Jotoardhi na Tanzania kutokana na eneo lake kubwa kupitiwa na Bonde la Ufa kuna uwezekano wa kupata umeme mwingi zaidi



*Kisima kifupi cha utafiti cha Jotoardhi kilichochoorongwa katika eneo la Kiejo-Mbaka wilayani Rungwe mkoani Mbeya.*



*Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba akifungua valvu ili kuruhusu majimoto yanayotoka ardhini kupita katika kisima kifupi cha utafiti cha Jotoardhi kilichochoorongwa katika eneo la Kiejo-Mbaka wilayani Rungwe mkoani Mbeya.*

## Megawati 200 za Jotoardhi kuzalishwa kabla ya mwaka 2025

unaotokana na nishati hiyo.

“Mfano hapa mkoani Mbeya katika eneo hili la Rungwe kumeonekana kuna uwezekano mkubwa wa kutoa nishati ya Jotoardhi kwa

sababu tawi moja la Bonde la Ufa limeingia katika eneo hili na Tawi jingine limeelekea upande wa Malawi.” Alieleza Mhandisi Mramba

Kwa upande wake,

Kaimu Meneja Mkuu wa Kampuni ya Uendelezaji wa Jotoardhi Tanzania (TGDC), Mhandisi Mathew Mwangomba alisema kuwa, eneo la Kiejo-Mbaka linaweza kuzalisha megawati 60 zinazotokana na Jotoardhi.

Alisema kuwa, Serikali imetoa takribani shilingi Bilioni 20 kwa ajili ya uendelezaji wa eneo hilo na sasa wamenunua mtambo wa kuchoronga

eneo hilo, na kwamba, Wataalam wa TGDC na Wahisani wameshirikiana katika kufanya tafiti zote zinazotakiwa.

Aliongeza kuwa katika eneo la Ngozi, inategemewa kuwa litazalisha megawati 70 zinazotokana na Jotoardhi na kwamba TGDC imejipanga vizuri katika kuhakikisha kuwa Tanzania inapata umeme kutoka kwenye nishati hiyo Jadidifu.



Watumishi mbalimbali kutoka Wizara ya Nishati na Kampuni ya Uendelezaji wa Jotoardhi Tanzania (TGDC) wakigusa majimoto yanayotoka katika kisima kifupi cha utafiti cha Jotoardhi kilichochoorongwa katika eneo la Kiejo-Mbaka wilayani Rungwe mkoani Mbeya. Wa Pili kutoka kulia ni Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba na wa kwanza kulia ni Kaimu Meneja Mkuu wa Kampuni ya Uendelezaji wa Jotoardhi Tanzania (TGDC), Mhandisi Mathew Mwangomba.

# Serikali inaendelea kusambaza Gesi Asilia majumbani - Mahimbali



Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Kheri Mahimbali (katikati) akipata maelezo ya matumizi ya gesi asilia ya kupikia kutoka kwa Mpishi Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Ufundi Mtwara Venant Makwinya (koti la bluu) wakati wa ziara ya kukagua miundombinu ya usambazaji wa gesi ya kupikia majumbani, Aprili 1, 2022, mkoani Mtwara.

## **Na Zueni Msuya, Mtwara**

Meelezwa kuwa, Serikali inaendelea na usambazaji wa miundombinu ya kusambaza Gesi asilia kwa matumizi ya kupikia majumbani na katika Taasisi mbalimbali zinazotoa huduma ya chakula kwa watu wake.

Hayo yalielezwa na Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Kheri Mahimbali wakati wa ziara yake ya kukagua usambazaji wa miundombinu ya Gesi asilia kwa matumizi ya kupikia majumbani na

katika Taasisi zinazotoa huduma ya chakula kama vile Shule na Magereza. Ziara hiyo aliifanya Aprili 1, 2022 mkoani Mtwara.

Katika ziara hiyo, Mahimbali alitembelea baadhi ya Taasisi zinazotumia gesi asilia kwa ajili ya kupikia ikiwamo Gereza la Lilungu, Shule ya Sekondari ya Mtwara pamoja na baadhi ya nyumba za wakazi wa Mtwara ambao tayari wameunganishwa na kutumia huduma hiyo.

Naibu Katibu Mkuu alitoa wito kwa wakazi wa Mtwara na maeneo yanayopitiwa na

miundombinu ya gesi kuchangamkia fursa hiyo kwa kuwa ni gharama nafuu ikilinganishwa na nishati nyingine ya kupikia.

Vilevile, alitembelea na kukagua Miundombinu ya kiwanda cha kuchakata Gesi Asilia cha Madimba pamoja na visima vya gesi vya vilivyopo eneo la Mnazi Bay pamoja kiwanda cha kuzalisha Saruji cha Dangote.

Kwa upande wake, Mkuu wa Wilaya ya Mtwara, Dunstan Kyobya aliwataka wawekezaji wa ndani wakiwemo wakazi wa Mtwara na nje ya nchi, kuwekeza katika mkoa huo kwa kuwa una nishati ya gesi ya kutosha.

Kyobya alishauri Taasisi zinazohusika na nishati hiyo, kuongeza kasi ya kutoa huduma ya kusambaza gesi hiyo



Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Kheri Mahimbali (katikati) akipata maelezo katika kituo cha kupunguza mgandamizo wa gesi kwa ajili ya matumizi ya majumbani, kilichopo nje ya gereza la Lilungu wakati wa ziara ya kukagua miundombinu ya usambazaji wa gesi ya kupikia majumbani, Aprili 1, 2022, mkoani Mtwara.

# Serikali inaendelea kusambaza Gesi Asilia majumbani - Mahimbali



*Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Kheri Mahimbali (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na uongozi wa gereza la Lilungu linalotumia gesi kupikia, wakati wa ziara ya kukagua miundombinu ya usambazaji wa gesi ya kupikia majumbani, Aprili 1, 2022, mkoani Mtwara.*

majumbani na katika taasisi zinatoa huduma ya chakula nchini ili kupunguza gharama za uendeshaji na kutunza mazingira.

Kwa mujibu wa

takwimu zilizotolewa na kampuni tanzu inayosimamia miundombinu ya gesi (GASCO) ya Shirika la Maendeleo ya Petrol (TPDC), ni kuwa,

wateja 425 katika mkoa huo wa Mtwara wameunganishwa na kutumia gesi asilia kwa ajili ya kupikia.

Wakizungumza wakati wa ziara hiyo, Mkuu wa Gereza la Lilungu Joseph Sabayo, pamoja na Mkuu wa Shule ya Sekondari Mtwara, Riyadh Kadhi wameishukuru Serikali kwa kuunganishiwa gesi asilia ya kupikia katika taasisi zao na kusema kuwa gesi hiyo imesaidia kupunguza gharama za matumizi ya fedha zilizokuwa zikitumika kununua kuni.

Kwa mujibu wa Mkuu wa Shule ya Sekondari Mtwara, Riyadh Kadhi, ni kuwa kwa Sasa

wanatumia shilingi Milioni 1.4 kwa mwezi kwa ajili ya kununua gesi ya kupikia shuleni hapo, ambapo awali walikuwa wakitumia shilingi Milioni Tatu mpaka Nne kwa ajili ya kununua kuni. Hivyo Gesi hiyo imeokoa takribani shilingi Milioni Mbili zilizokuwa zikitumika kununua kuni.

Kadhi alisema kuwa matumizi ya Gesi pia yamerahisisha na kupunguza muda wa kuandaa chakula kwa wanafunzi wa shule hiyo na pia imeweka mazingira rafiki kwa wapishi wanapotekeleza majukumu yao.



*Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Kheri Mahimbali akitazama mita zinazoonisha ujazo wa gesi inayoingia kwenye magari yanayotumia gesi katika kiwanda cha kuzalisha Saruji cha Dangote, wakati wa ziara ya kukagua miundombinu ya usambazaji wa gesi ya kupikia majumbani, Aprili 1, 2022, mkoani Mtwara.*



Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Kheri Mahimbali, (wa pili kulia) akikagua eneo Ila Mnazi Bay lenye visima vya kuzalisha gesi asilia, wakati wa ziara ya kukagua miundombinu ya usambazaji wa gesi ya kupikia majumbani, Aprili 1, 2022, mkoani Mtwara.



Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Kheri Mahimbali akisaini kitabu cha wageni katika kiwanda cha kuchakata gesi asilia cha Shirika la Maendeleo ya Petrol Tanzania (TPDC), Madimba wakati wa ziara ya kukagua miundombinu ya usambazaji wa gesi ya kupikia majumbani, Aprili 1, 2022, mkoani Mtwara.



Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Kheri Mahimbali (kushoto) na Mkuu wa Wilaya ya Mtwara Dunstan Kyobya wakibadilishana mawazo, wakati wa ziara ya kukagua miundombinu ya usambazaji wa gesi ya kupikia majumbani, Aprili 1, 2022, mkoani Mtwara.



Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Kheri Mahimbali, (katikati) akitoa maelekezo kwa ujumbe alioambatana nao wakati wa ziara ya kukagua miundombinu ya usambazaji wa gesi ya kupikia majumbani, Aprili 1, 2022, mkoani Mtwara.



Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Kheri Mahimbali, akikagua kifaa kinachotumika kujaza gesi kwenye magari inayotumika kuendesha magari, wakati wa ziara ya kukagua miundombinu ya usambazaji wa gesi ya kupikia majumbani, Aprili 1, 2022, mkoani Mtwara.



# Visima vya nishati ya Jotoardhi kuanza kuchorongwa Songwe



Picha ya pamoja kati ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba (Wa Sita kushoto) na Wafanyakazi wa Kampuni ya Uendelezaji wa Jotoardhi Tanzania (TGDC), TANESCO pamoja na wakazi wa Kijiji cha Nanyala katika eneo ambalo utafanyika uchorongaji wa kisima cha Jotoardhi ambapo mategemeo yake ni kupata Megawati 5 – 38 za Umeme wa Jotoardhi.

megawati 5 ifikapo mwaka 2023.

Hayo yalisemwa tarehe 15 Aprili, 2022 wakati wa ziara ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba katika eneo utakapotekelezwa mradi huo wa Jotoardhi katika Kijiji cha Nanyala wilayani Mbozi, Mkoa wa Songwe.

Mhandisi Mramba alieleza kuwa, lengo la ziara hiyo lilikuwa ni kujionea hali ya eneo hilo, hatua zilizofikiwa hadi sasa za uendelezaji wa rasilimali hiyo ya Jotoardhi pamoja na hatua zinazopaswa kuchukuliwa ili kuhakikisha mradi huo unatekelezwa ili kuweza kupata umeme kutokana na nishati hiyo.

Alisema kuwa, Serikali imejikita katika

meelezwa kuwa, Kampuni ya Uendelezaji Jotoardhi Tanzania (TGDC) kuanzia mwezi Mei

mwaka huu itanza kuchoronga visima vifupi vya utafiti katika mradi wa Jotoardhi Songwe, vitakavyosaidia

kupata taarifa za uhakika za kisayansi zitakazowezesha mradi huo kuanza kuzalisha umeme wa kiasi cha



Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Eng. Felchesmi Mramba akisisitiza jambo wakati wa ziara yake katika eneo la uendelezaji wa Jotoardhi mkoani Songwe. Kulia kwake ni Kaimu Meneja Mkuu wa Kampuni ya Uendelezaji Jotoardhi Tanzania (TGDC), Mhandisi Mathew Mwangomba na kushoto kwake ni Mhandisi Shakiru Idrissa, Mkurugenzi wa Maendeleo ya Biashara kutoka TGDC.



Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Eng. Felchesmi Mramba (katikati) akikagua eneo lenye nishati ya Jotoardhi katika Kijiji cha Nanyala wilayani Mbozi mkoani Songwe. Kulia kwake ni Kaimu Meneja Mkuu wa Kampuni ya Uendelezaji Jotoardhi Tanzania (TGDC), Mhandisi Mathew Mwangomba na kushoto kwake ni Mhandisi Shakiru Idrissa, Mkurugenzi wa Maendeleo ya Biashara kutoka TGDC.

# Visima vya nishati ya Jotoardhi kuanza kuchorongwa Songwe

kuendeleza nishati Jadidifu ambazo ni endelevu, salama na rafiki wa Mazingira kama vile Jotordhi ili kuhakikisha kuwa kunakuwa na uhakika wa uzalishaji umeme nchini kwani nishati nyingine kama vile Gesi Asilia ambayo inazalisha umeme kwa kiasi kikubwa kwa sasa nchini huwa inaisha tofauti na nishati jadidifu kama ya Jotoardhi.

Aidha, alielekeza kuwa, wakati TGDC ikiwa kwenye mpango wa kuanza kuchoronga visima vya majaribio na vya kuzalisha mvuke,

wanapaswa kuwa na hatimiliki ya eneo hilo ili kuwa na uhakika na eneo hilo ambalo lina manufaa makubwa kwa nchi.

Vilevile aliipongeza TGDC kwa kuwa tayari imeanza kujipanga na uendelezaji wa eneo la mradi ikiwemo uwepo wa viwanda mbalimbali kama vile vinavyohitaji Joto na Majimoto ili kutekeleza za uzalishaji na hivyo aliwaasa wananchi wa Kijiji hicho cha Nanyala kuendelea kutunza eneo hilo litakalokuwa na manufaa.

Awali, Kaimu Meneja Mkuu wa TGDC, Mhandisi

Mathew Mwangomba, alimweleza Katibu Mkuu kuwa, mradi huo ulianza kutekelezwa mwaka 2018 na unatarajiwa kukamilika mwaka 2023/24 ukiwa na uwezo wa kuzalisha umeme wa kiasi cha megawati 5 hadi 38.

Alisema kuwa, pamoja na kujipanga na kuanza kazi ya kuchoronga visima, TGDC inaendelea na utekelezaji wa miradi ya matumizi mengine katika eneo la mradi ikiwemo kuongeza thamani ya mazao ya mifugo ambapo kutajengwa mabwawa ya kufugua Samaki

pamoja na teknolojia ya kutotolesha vifaranga vya kuku kwa kutumia Jotoardhi.

Aliongeza kuwa, miradi mingine inayoendelea kutekelezwa kutokana na uwepo wa nishati ya Jotoardhi ni pamoja na uendelezaji wa kilimo ambapo kutajengwa nyumba kitalu kuongeza thamani ya mazao ya kilimo kama kukausha mazao kwa kutumia joto na kuboresha vivutio vya utalii vinavyopatikana katika maeneo ya Jotoardhi kama vile bwawa la kuogelea la majimoto.

Tanzania ina uwezo wa kuzalisha umeme wa Jotoardhi usiopungua megawati 5000 zinazopatikana ndani ya mikoa 16 nchini.



Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Eng. Felchesmi Mramba (katikati) akitazama maji ya moto yanayotoka ardhini katika Kijiji cha Nanyala wilayani Mbozi mkoani Songwe ikiwa ni moja ya ishara za uwepo wa nishati ya Jotoardhi katika eneo hilo. Kulia kwake ni Kaimu Meneja Mkuu wa Kampuni ya Uendelezaji Jotoardhi Tanzania (TGDC), Mhandisi Mathew Mwangomba na kushoto kwake ni Mhandisi Shakiru Idrissa, Mkurugenzi wa Maendeleo ya Biashara kutoka TGDC.



Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Eng. Felchesmi Mramba (wa Pili kulia) akipata maelezo kutoka kwa Kaimu Meneja Mkuu wa Kampuni ya Uendelezaji Jotoardhi Tanzania (TGDC), Mhandisi Mathew Mwangomba (wa Pili kushoto) kuhusu kifa cha ukusanyaji wa taarifa za Jotoardhi kilichofungwa katika eneo lenye nishati ya Jotoardhi katika Kijiji cha Nanyala wilayani Mbozi, Mkoa wa Songwe. Wa kwanza kulia ni Mhandisi Shakiru Idrissa, Mkurugenzi wa Maendeleo ya Biashara kutoka TGDC.

## Naibu Katibu Mkuu Nishati akagua eneo la mradi wa LNG



Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Kheri Mahimbali (wa kwanza kushoto), akitoa maelekezo kwa Watendaji wa Wizara hiyo na Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), alipowasili katika eneo litakalojengwa mradi wa kusindika Gesi Asilia (LNG), Likong'o Mkoani Lindi Aprili, 02, 2022.

### Na Zueni Msuya, Lindi

**N**aibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Kheri Mahimbali ametembelea na kukagua eneo la

Likong'o litakalojengwa Mradi wa kusindika Gesi Asilia (LNG) na eneo la makutano ya kuunganisha gesi inayotoka mkoani Mtwara na Songosongo mkoani Lindi.

Akiwa katika ziara hiyo aliwaasa watendaji kutekeleza majukumu

yao kwa weledi ili miradi hiyo ilete manufaa kwa wananchi na taifa kwa ujumla.

Katika ziara hiyo, Mahimbali aliambatana na Mkuu wa Wilaya ya Lindi, Shaibu Ndemanga, Kamishna Msaidizi wa Mafuta na Gesi kutoka Wizara ya Nishati, Mhandisi Mohamed Fasih, Meneja wa Kiwanda cha kuchata gesi asilia cha Madimba, Mhandisi Sultan Pwaga, pamoja na maafisa wengine kutoka wizarani na Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC). Ziara hiyo ilifanyika Aprili 2, 2022 mkoani Lindi.

Ziara hiyo ni muendelezo wa ziara yake aliyoianza Machi 31, 2022 kwa kukagua mradi wa gesi wa Songosongo mkoani Lindi, kisha Aprili 1, 2022 alikagua kiwanda cha kuchakata gesi asilia cha Madimba, visima vya gesi katika eneo la Mnazi Bay pamoja mradi wa usambazaji wa miundombinu ya gesi asilia kwa matumizi ya kupikia majumbani.



Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Kheri Mahimbali (kulia) akionyesha mchoro wa ramani ya eneo litakalojengwa mradi wa kusindika gesi asilia (LNG na Mjiolojia mwandamizi wa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), Simon Zabron, wakati wa ziara ya kukagua eneo hilo lililopo Likong'o Mkoani Lindi, Aprili, 02, 2022.



*Kamishna Msaidizi wa Mafuta na Gesi wa Nishati kutoka Wizara ya Nishati, Mhandisi Mohammed Fakhifafanua jambo kwa Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Kheri Mahimbali (wa pili kulia), wakati wa ziara ya kukagua eneo hilo lililopo Likong'o Mkoani Lindi, Aprili, 02, 2022.*




*Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Kheri Mahimbali, akikagua sehemu ya mabomba ya gesi asilia katika kituo cha makutano ya kuunganisha gesi hiyo inayotoka Mtwara na Songosongo Mkoani Lindi, mara baada ya kutembelea kituo hicho kilichopo katika Kijiji cha Somangafungu Mkoani Lindi Aprili, 02, 2022.*



*Muonekano wa sasa wa eneo litakalojengwa mradi wa kusindika gesi asilia (LNG) lililopo Likong'o Mkoani Lindi.*

# JARIDA HILI LA MTANDAONI HUTOLEWA NA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI, WIZARA YA NISHATI



**Fika Ofisi ya Mawasiliano,**  
Mji Mpya wa Serikali Mtumba, S.L.P. 2494, Dodoma au  
Wasiliana nasi kwa **simu namba** +255-26-2322018  
**Nukushi** +255-26-2320148

 [www.nishati.go.tz](http://www.nishati.go.tz)

 [Wizara ya Nishati](https://www.facebook.com/Wizara.ya.Nishati)

 [@Nishati2017](https://twitter.com/Nishati2017)

 [wizara\\_ya\\_nishati\\_tanzania](https://www.instagram.com/wizara_ya_nishati_tanzania)

 [Wizara ya Nishati](https://www.youtube.com/Wizara.ya.Nishati)